16:29-22:53 HUDUMA YA ELIYA

Ubaali wa Yezebeli katika Israeli (16:29-17:24)

Ahabu, mfalme mpya wa Israeli alifanya mapatano ya ushirikiano na mfalme Ethbaali ambaye pia alikuwa kuhani wa nchi ya Sidoni (yaani Foiniki), akamwoa Yezebeli binti yake. Licha ya kupokea dini ya Baali ya mkewe, Ahabu pia aliweka dini hiyo kuwa ya kitaifa, akajenga hekalu la Baali katika mji mkuu wa Israeli, Samaria (16:29-33). Dini hiyo ya Baali iliyoingizwa na Yezebeli ilikuwa ya aina mbaya na yenye hatari zaidi kwa dini ya Israeli kuliko dini ile ya kawaida ya Baali ya Wakanaani iliyoendeshwa katika sehemu mbalimbali za vilele vya milima. Ubaali ulioingizwa na Yezebeli (tunauita Ubaali wa Yezebeli ili kuutofautisha na ule wa kawaida), ulikuwa ule wa Mungu mkubwa Melkarti (au Melqart) ambaye makao yake makuu yalikuwa nyumbani kwao Yezebeli, yaani katika mkoa wa Foiniki wa Tiro na Sidoni. Hatimaye Yezebeli alifanya bidii kuingiza dini hiyo iwe dini rasmi ya Israeli.

Tabia ya kumwasi Mungu katika nchi yote wakati ule ilionekana wazi katika kujengwa upya kwa mji wa Yeriko. Jambo hilo lilikuwa kinyume kabisa cha amri ya Mungu (34; taz.Yos 6:26).

Wakati ule ulikuwa wa hatari sana kwa dini ya Israeli, hata Mungu alipaswa kutumia miujiza na hukumu kali ili kuzuia mambo yale. Kwanza alimtuma nabii Eliya ili atangaze ukame wa miaka mitatu na nusu katika nchi yote (17:1). Jambo hili lilionyesha udhaifu wa Baali, ambaye aliaminiwa kuwa mungu wa hali ya ulimwengu na wa ustawi wa mimea na mifugo. Wakati huo huo nguvu ya BWANA ilionekana ambaye bado akiendelea kuwa Mungu wa kweli wa Israeli. Bila shaka nabii Eliya hakupendwa na watu wengi kwa sababu ya ukame ule. Hivyo Mungu alimwongoza ajifiche karibu na mto fulani katika nchi ya nyumbani kwao Gileadi, mashariki mwa Yordani. Maficho yake hayakujulikana naye hakuwa na haja ya kutoka ili atafute mahitaji, kwa sababu Mungu alimpa riziki yake kwa njia ya miujiza (2-6).

Maji ya mto ule yalipokauka (7), Mungu alimtuma Eliya Zarepta katika nchi ya Sidoni (Foiniki). Nchi ile ilikuwa na makao makuu ya Baali, lakini ukame wa huko ulikuwa mkali kama ulivyokuwa Israeli. Miujiza ya kulishwa kwa Eliya pamoja na ile ya nyumbani mwa mjane yule ilionyesha kwamba nguvu ya Mungu ilikuwa kubwa kuliko ile ya Baali, hata katika nchi yenyewe ya Baali, nayo haikutegemea hali au kanuni za ulimwengu kama Baali. Matukio yale pia yanaonyesha kwamba imani, wala siyo ukabila ni msingi wa baraka ya Mungu (8-16; taz.Lk 4:25-26). Uponyaji wa mwana wa mjane ulithibitisha imani yake kwa Mungu, nayo ilimhakikishia Eliya kuwepo kwa nguvu ya Mungu hata katika siku za ukiwa na hatari zilizomkabili (17-24).

Eliya na manabii wa Baali (18:1-46)

Hali ile ya ukame iliendelea kwa mfululizo wa mihula mitatu, ndipo Mungu alipomwambia Eliya kwamba wakati huo mfalme Ahabu pamoja na Waisraeli wote wapate nafasi ya kuamua, wamfuate Baali au BWANA (18:1-2). Ahabu alihangaika na matokeo ya ukame kwa ajili ya biashara ya Israeli na usalama wa nchi (kwa sababu aliogopa farasi na nyumbu zake wangekufa), wata hakujali sana hali ya dini ya nchi yake. Bado aliendelea kujaribu kumtumikia BWANA na Baali pia. Malkia Yezebeli alipojaribu kuwashambulia manabii wa BWANA, afisa mkubwa aliyemcha Mungu aliwahifadhi na kuwalisha (3-6).

Eliya aliporudi Israeli alitaka kumwona Ahabu (7-16). Alimweleza Ahabu wazi kwamba kugawanya uaminifu kati ya BWANA na Baali, machoni pa BWANA kulikuwa kumwasi Yeye, na dhambi hiyo ya Ahabu ndiyo iliyosababisha taabu ile ya Israeli yote (17-18).

Yezebeli alifanya bidii sana kuimarisha ibada ya Baali, hata wakati huo alikuwa na manabii wa Baali wengi sana, mamia kwa mamia waliomfanyia kazi. Eliya alimchokoza Ahabu ili awaalike manabii wote wa Baali waje katika Mlima Karmeli (mlima ule ulikuwa eneo rasmi la Baali), ili huko ionekane hadharani Mungu yupi alikuwa wa kweli, Baali au BWANA (19-24). Baali aliaminiwa kuwa mungu wa hali ya hewa, lakini alionyeshwa kuwa hana uwezo (25-29). BWANA alijidhihirisha kuwa mwenye mamlaka yote juu ya hali ya hewa na ya ulimwengu wote, akimshinda Baali katika ushindi mkubwa ulioleta mvua na radi, maji na moto (30-39). Watu walipotambua ushindi wa BWANA, Eliya alitumia nafasi hiyo ili kuwaangamiza manabii wa Baali (40).

Eliya alithibitisha mara ya mwisho kwamba Mungu ndiye atawalaye hali ya hewa na ya ulimwengu, wala si Baali, alipotangaza hadharani kwamba kuanzia wakati huo ukame ungekwisha. Ahabu alipokimbiza gari lake kwenda nyumbani ili akimbie mvua kali iliyokaribia, Eliya, akiwa na

nguvu ya Mungu, alipiga mbio mbele yake kwa furaha ya ushindi (41-46).

Mungu ampa Eliya matumaini mapya (19:1-21)

Yezebeli aliposikia kwamba Eliya aliwaua manabii wake, alitishia kumfanyia Eliya vivyo hivyo. Yezebeli bado alikuwa na mamlaka makubwa juu ya watu ambao, ijapokuwa waliona ushindi mkubwa wa Eliya katika Mlima Karmeli, mara walirudia ibada yao ya miungu (19:1-2,10). Eliya akatoroka kwenda nchi ya ukame kusini mwa Yuda. Huko alikuwa katika hali ya kuchoka na kukata tamaa akatamani kufa. Lakini kwa njia ya kumlisha chakula cha mwujiza, Mungu alimwezesha kwenda kusini kabisa mpaka alipofika katika Mlima Horebu wa Sinai, ambapo hapo awali Mungu aliwapa watu wake sheria na agano (3-8).

Eliya alitambua kwamba Waisraeli hawakuguswa sana mioyoni mwao, si kutokana na taabu ya ukame, wala si kwa kuondolewa kwa ukame huo kwa njia ya ishara kubwa, hivyo alifikiri kwamba agano la Musa halikuwa na maana sana kwao (9-10). Kwa hiyo Mungu alimwonyesha kwamba, ingawa matukio ya nguvu na ishara yanasaidia kidogo tu, faida ya kweli na ya kudumu kwa manufaa ya kiroho na imani vinatokana na jambo moja tu, yaani kama watu wanasikiliza sauti ya Mungu mioyoni mwao na kuitikia inavyopaswa (11-14). Kwa njia ya kazi ya mfalme Hazaeli wa Dameski, aliyekuwa adui wa Israeli, kwa mfalme Yehu wa Israeli na kwa nabii Elisha matukio ya ishara yangetokea na kuwaadhibu Waisraeli, lakini siku zote wangekuwepo watu wachache ambao wangetii sauti ya Mungu na kudumu kuwa waaminifu kwake (15-18).

Hali amepewa matumaini mapya, Eliya alirudi Israeli. Elisha alionyesha kwamba alikuwa tayari kuendeleza kazi ya Eliya alipochinja ng'ombe zake (waliokuwa tegemeo la riziki yake), na kuwaandalia jamaa na marafiki zake karamu ya kuagana nao (19-21).

Kushindwa kwa Ben-hadadi (20:1-43)

Ahabu alionekana kuwa na shida sana jeshi la Shamu (Syria) pamoja na majeshi mengine ya jirani yalipozingira mji mkuu wa Samaria kivita, na kudai fedha nyingi sana. Mwanzo Ahabu alikubali (20:1-4), lakini walipoongeza madai yao, Ahabu aliamua kupigavita (5-12).

Nabii mmoja alimhakikishia Ahabu kwamba Mungu angewapa Waisraeli ushindi (13-15). Mpango wa Ahabu uliofuatana na ushauri wa nabii ulikuwa hivi: Kwanza atume kundi kubwa la vijana ili wawachokoze Washami, kisha jeshi lake rasmi lifuate na kuwashambulia maadui ghafla. Ahabu alipata ushindi mkubwa, lakini alionywa kwamba ajihadhari na mashambulio mengine ya muhula wake (16-22).

Washami waliongeza na kuimarisha majeshi yao, wakiwaondoa viongozi wa wafalme wadogo na kuweka maakida wao wenyewe wenye uzoefu wa vita. Pia walifikiri kwamba wangepata bahati zaidi ya ushindi, kama wangebadili mahali pa vita na kupiga vita vyao katika eneo ambapo miungu yao ingekuwa na nguvu zaidi. Waisraeli wakashinda tena, na hivyo Mungu aliwathibitishia Washami (na hata Ahabu) kwamba ilikuwa kosa kubwa kufikiri kwamba nguvu ya Mungu ilikuwa haba na kutegemea mahali fulani tu (23-30).

Ahabu alimkamata mfalme wa maadui, Ben-hadadi, lakini alimwacha huru tena baada ya kupatana naye kurudishiwa eneo la Israeli ambalo lilitekwa na Washami hapo awali. Wafalme hao wawili pia walifanya mapatano yenye faida kubwa kwa Israeli. Labda mapatano yale na Shamu yalikuwa na makusudi ya kuongeza nguvu za nchi mbili hizo dhidi ya maadui wengine ambao wangeweza kushambulia nchi zao. Lakini mapatano yale yasingekuwa lazima, kama Ahabu angemtegemea Mungu, alivyoonyeshwa katika ushindi wake wa awali kidogo (31-34). Nabii kijana alimwonyesha Ahabu kwa mfano wa maigizo kwamba, kwa kuwa hakutumia nafasi aliyopewa na Mungu ya kumwangamiza adui kabisa, adui yule yule angerudi na kusababisha taabu nyingi kwa Waisraeli (35-43).

Shamba la mizabibu la Nabothi (21:1-29)

Tumekwisha ona kwamba siasa yote ya Ahabu kuhusu dini, jeshi na biashara ilikuwa kinyume cha mapenzi ya Mungu. Mbinu aliyotumia ili kujipatia shamba la mizabibu la Nabothi, inaonyesha wazi kwamba hata katika mambo ya haki ya kiraia hakujali sheria ya Mungu. Mwanzo Ahabu alikubali kumpa Nabothi bei nzuri kwa shamba lake. Nabothi akakataa kwa sababu mashamba yaliyokuwa urithi kutoka kwa wazazi, na katika sheria ya Israeli yalikuwa mali ya thamani sana isiyoweza kuuzwa (21:1-4). Kwa hiyo Yezebeli alifanya njama dhidi ya Nabothi ili ashtakiwe kwa uongo na kuuawa. Ilikuwa rahisi kuwahonga watu. Mahakimu wa mahakama ndogo walipokea rushwa, wala hakuwepo mtu katika Israeli aliyeweza kutetea haki ya raia wa hali ya kawaida (5-16).

Ahabu alipochukua shamba la Nabothi, alikutana na Eliya. Nabii huyo akatabiri hukumu ya Mungu juu ya Ahabu na hasa juu ya mkewe Yezebeli aliyejaa tamaa ya uuaji (17-24). Baada ya utawala wa wana wa Ahabu, ufalme wa nasaba ya Omri ungefikia mwisho wake (25-29).

Ahabu na Yehoshafati (22:1-40)

Miaka mitatu baada ya kufanya mapatano na mfalme Ben-hadadi, Ahabu alivunja mapatano hayo. Aliona nafasi ya kutwaa mji wa mpakani wa Ramoth-gileadi, naye alimshawishi Yehoshafati, mfalme wa Yuda, amsaidie (22:1-4). (Muda mfupi kabla ya mambo hayo, Yehoshafati alikuwa amefanya mapatano na Ahabu, akimwoza mwanawe Yehoramu na binti wa Ahabu, Athalia; 2Fal 8:16-18,25-26; 2Nya 18:1.)

Manabii wenye cheo walioajiriwa na Ahabu walitafuta kumpendeza mfalme wao kuliko kumwambia mapenzi ya Mungu. Yehoshafati hakuridhika na utabiri wao, akamwomba Ahabu amwite nabii mwingine, yaani Mikaya (5-12).

Mikaya aliyeonywa na mjumbe aliyemwita ili akubaliane na manabii walioajiriwa, alikariri maneno yao tu, lakini hata Ahabu aliona kwamba Mikaya hakusema maneno aliyoyaamini mwenyewe (13-16). Hatimaye Mikaya akaamua kutabiri ukweli wa Mungu wazi: Manabii walisema uongo, na Israeli ingeshindwa (17-23). Nabii mmojawao wa wale walioajiriwa alipopinga neno la Mikaya la kuwalaumu manabii wengi, yeye Mikaya alijibu kwamba alitumia wakati mwingi ili kutafuta mapenzi ya Mungu, kuliko kusema maneno ya bure tu ya kumpendeza mfalme. Mfalme akaitikia neno lile la kumlaumu Mikaya akamfunga gerezani (24-28).

Kwa kiburi na ujinga wake Ahabu hakujali unabii wa Mikaya akaenda kuchokoza vita na Shamu. Ujanja wake wa kukwepa kuuawa kwa njia ya kuvaa kama askari wa kawaida haukumsaidia. Alijeruhiwa katika mwanzo wa vita, lakini alijikaza kutwa nzima ili kuwahimiza watu wake, akafa usiku ule ule (29-36). Unabii wa Eliya ukaanza kutimizwa (37-40; taz.21:19).

Matendo mema ya Yehoshafati (22:41-53)

Ingawa wafalme Asa na Yehoshafati walileta marekebisho mengi ya dini katika Yuda, ibada ya Mabaali katika vilele vingine vya milima haikuondolewa kabisa nchini. Hata hivyo, Yehoshafati alitaka kurekebisha mambo mengi katika Yuda. Alikusanya kundi la makuhani, Walawi na maafisa wa serikali, akawatuma nchini kote ili wafundishe sheria ya Mungu (41-43; 2Nya 17:1-9). Pia aliimarisha jeshi la Yuda kiasi kwamba mataifa ya jirani yakaona vema kutafuta urafiki naye (2Nya 17:10-19). Mambo mengine yaliyosifiwa katika utawala wake yalikuwa marekebisho ya sheria na haki ya mahakama na ushindi wake wa ajabu juu ya jeshi kubwa la maadui kwa njia ya kumwamini Mungu tu (taz.maelezo ya 2Nya 19:4-20:30).

Ujinga wa Yehoshafati wa kufuatana na Ahabu kwenda vitani uliharibu sehemu ya sifa nzuri ya utawala wake mwema (44-46; 2Nya 19:1-3). Kufuatana na siasa yake ya kupatana na Israeli, aliamua kujiunga na mwana wa Ahabu kwa kuendesha meli za biashara. Meli zile zilipoharibika, Yehoshafati alitambua kwamba nabii aliyemwonya kabla ya mambo hayo alisema kweli kwamba haikuwa mapenzi ya Mungu yeye aendelee kushirikiana na mfalme mwovu Ahazia (47-53; 2Nya 20:35-37).